



TAARIFA KWA UMMA

UTEKELEZAJI WA MASHARTI YA LESENI ZA USAFIRISHAJI MABASI YA MASAFA MAREFU

Kwa mujibu wa Kifungu Na 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, Mamlaka pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara.

Katika kutekeleza jukumu hilo, tarehe 1 June, 2022 Mamlaka ilianza rasmi kuthibitisha madereva wa vyombo vya moto kibiashara. Aidha, moja ya masharti ya leseni zinazotolewa na LATRA ni wenyewe vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara, kuhakikisha madereva wanaoendesha vyombo hivyo wanakuwa na Cheti cha Uthibitisho kinachotolewa na Mamlaka baada ya kufanya mtihani na kufaulu.

Sharti la leseni kwa mtoa huduma za usafiri wa abiria kutumia dereva mwenye cheti cha uthibitisho kinachotolewa na Mamlaka, limeainishwa kwenye Kanuni ya 22(i) ya Leseni za Usafirishaji (Magari ya Abiria), 2020. Kutokana na takwa hilo la kisheria, Mamlaka inawatangazia wamiliki wote wa mabasi kuhakikisha madereva wao wote wamesajiliwa ifikapo tarehe 30 Aprili, 2023. Usajili unafanyika kwenye ofisi zote za LATRA Tanzania Bara na hivyo madereva wote waelekezwe kufika kwenye ofisi za LATRA ili waweze kusajiliwa.

Kwa madereva watakaoshindwa kufika kwenye ofisi za LATRA wanaweza kutuma maombi ya kusajiliwa kupitia anuani ya <https://rrims.latra.go.tz/login>. Maombi ya kusajiliwa yaambatishwe **Leseni ya udereva, Cheti cha taaluma ya udereva kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali na Taarifa ya Uthibitisho wa afya kutoka Hospitali ya Serikali**. Fomu ya Uthibitisho wa Afya inapatikana kwenye tovuti www.latra.go.tz na ofisi za LATRA.

Imetolewa na:

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano

17 Februari, 2023